

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

SHULE YA SEKONDARI LWANGWA,
S.L.P 131,
TUKUYU.
11/06/2023

KUMB. NA. LWS/JO/VOL.1/04

Mkuu wa shule: 0744154630/0682196619
Makamu Mkuu Wa shule: 0765521643/0755300906
Mhasibu: 0621247302/0762016908
Patron: 0624147029
Matron: 0768455555

Mzazi/mlezi wa mwanafunzi

.....
S.L.P

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI LWANGWA.
Ninayo furaha kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano Tahasusi (Combination)katika shule hii katika mwaka wa masomo 2023/2024 shule itafunguliwa tarehe 14/08/2023. **Mwisho wa kuripoti tarehe 31.08.2023**

Lwangwa sekondari ni shule ya serikali, shule hii ni ya kutwa kwa kidato cha I-IV na Bweni kwa kidato cha V – VI iko mkoa wa Mbeya, wilaya ya Rungwe Halmashauri ya Busokelo umbali kilometra 41 kutoka Tukuyu mjini.

MAHALI SHULE ILIPO

Unaweza kufika shuleni kwa kutumia usafiri wa namna mbili kama ifuatavyo:

- (i) Unaweza ukatumia basi linaitwa **SIKUTEGEMEA, MAJAHÀ, NA MAGOMA** mabasi hayo yanaanza safari saa 3:30 asubuhi kutoka Mbeya kuelekea Lwangwa ambayo yanapatikana stendi ya Nanenane mjini Mbeya. Ukiyakosa mabasi hayo unaweza kupanda **COSTA** kutoka mbeya mjini hadi Tukuyu mjini shuka uliza stendi ya Lwangwa. Nauli yakutoka Mbeya mpaka Lwangwa kwa basi ni Tsh. 8,000/= na kutoka Mbeya mpaka Tukuyu ni Tsh. 4,000/= na kutoka Tukuyu mpaka Lwangwa ni Tsh. 6,000/= kwa gari aina ya Noah.

MAAGIZO

2.1. SARE NA VIFAA VINGINE

1. (A) WAVULANA

Suruali 03 dark blue 1 gold 1 na kijivu1 zote kitambaa estem namba 1 zenyetanapu na upana chini nchi 16

(Duck blue ishonwe nyumbani gold na kijivu zitashonwe shuleni ili kuepusha kukosea rangi).

(B) WASICHANA

Sketi 03 dark blue1 gold 1 na kijivu 1 zote kitambaa estem namba 1 zenyemalinda ya kawaida urefu kifundo cha mguu. (dark blue ishonwe nyumbani na shamba dress gauni rangi ya maruni solo ndefu ya mikono mirefu, gold na kijivu zitashonwa shuleni ili kuepusha kukosea rangi.

2. Mashati meupe mawili mikono mirefu.
3. Viatu vyeusi vya kamba visivyo na kisigino kirefu
4. Soksi nyeusi kwa wavulana na wasicha na nyeupe ndefu.
5. Sweta rangi ya kijani jeshi yenye shingo umbo la V (kuepusha kuchanganya rangi tunashauri uje anunue huku shuleni)
6. Aje na jaketi jeusi nje na ndani sio koti
7. Aje na kwanja 1 lililonolewa, Jembe 1, Mopa 1 au Blash ndefu na Fagio la Chelewa kwa ajili ya kufanya usafi.
8. Aje na ndoo kubwa moja kwa ajili ya matumizi ya shule na ndogo kwa ajili ya matumizi binafsi.
9. Aje na godoro nchi $2 \frac{1}{2}$ X 6 pia yanapatikana Lwangwa madukani
10. Aje na shuka jozi mbili rangi ya pinki moja na blue bahari moja
11. Aje na mto na foronya mbili rangi ya Pinki moja na Blue moja
12. Aje na blacketi zito kwa ajili ya kujistili na baridi
13. Aje na chandarua kimoja
14. Aje na taulo moja
15. Aje na mswaki, dawa ya meno na sabuni (pia vinapatikana kwenye duka la shule)
16. Aje na sahani (Container), kijiko na kikombe kwa ajili ya chakula (chakula kinatolewa shuleni)

NB: anapo kuja kuripoti mwanafunza awe amevaa sare za shule (track au dark blue na haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani.)

Pia mwanafunzi asishone suruali inayobana (modo) au sketi fupi adhabu kali itachukuliwa kwa mwanafunzi atakae kiuka maagizo hayo.

2.2. VIFAA VYA MICHEZO

- a) Bukta na fulana rangi ya Blue kwa ajili ya michezo isiyo na michoro wala maandishi
- b) Soksi jozi moja ndefu
- c) Track rangi ya blue
- d) T-shirt yenye nembo ya shule zitapatikana shulenii
- e) Raba za michezo (hivi vifaa ni kwa wanafunzi wote)

2.3. VIFAA VYA MASOMO

Unatakiwa kuleta vifaa vya masomo kama ifuatavyo

- ❖ Madaftari makubwa (Counter book 7 kwa artist na 10 kwa michepuo mingine)
- ❖ Scientific calculator FX 991 kwa wanafunzi wa sayansi na Biashara
- ❖ Karamu za wino blue au nyeusi na za risasi
- ❖ Mkebe (Mathematical set)
- ❖ Four figure table au mathematical table.
- ❖ Vitabu vya kujisome mwanafunzi kwa masomo husika
- ❖ Ream 1 A4 iletwe shulenii
- ❖ Aje na kamusi ya Kiswahili, kiingereza (Oxford Advanced learners Dictionary) kwa mwanafunzi wa michepuo wa HGL, HGE na HGK.

2.4 FEDHA

- i. Mchango wa Uendeshaji wa Shule Tsh. 65,000/=
- ii. Tahadhari Tsh. 5,000/=
- iii. Nembo Tsh. 5,000/= kwa mwaka
- iv. Kitambulisho Tsh. 5,000/=

NB: Jumla ya michango yote ni Tsh. 80,000/= inalipwa kwa awamu mbili anapo ripoti Tsh. 40,000/= 2023 awamu ya pili ni januari 2024 Tsh. 40,000/= .

Fedha zote zilipwe Benki A/C NA. **61403500101 NMB (LWANGWA SEKONDARI SCHOOL REVENUE COLLECTION ACCOUNT)** aje na orginal payslip. Isipo kuwa fedha za matibatu na usafiri hizo zisilipwe kwenye akaunti ambayo ni (Kama hana Bima ya Afya) Tsh. 7,000/= kwa ajili ya bima ya (CHIF).

2.5. KABLA YA KUFIKA SHULENI ZINGATIA YAFUATAYO

- i. Kupimwa afya tumia fomu iliyoambatanishwa, pia Hospitali ya serikali
- ii. Aje na cheti cha kuzaliwa (Nakala) au affidavit ambayo inapatikana mahakama ya wilaya
- iii. Kusoma na kuzielewa sheria/ kanuni za shule zimeambatanishwa
- iv. Kujaza fomu ya taarifa binafsi iliyoambatanishwa
- v. Kuhakikisha kuja na result slip kwa ajili ya kusajiliwa bila hivyo huta pokelewa wala kusajiliwa.

- vi. Hakikisha malipo yote yamefanyika kikamilifu.
- vii. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na simu shuleni

2.6. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Mwanafunzi atatakiwa kufuata na kutekeleza sheia na kanuni zote za shule kama inavyotakiwa. Hongera kwa kupata nafasi hii ya pekee kati ya wanafunzi waliofanya vizuri.

Ukifika shuleni zingatia kilichokuleta shule hii ni kujifunza na kuelimika. Hivyo unatakiwa kudumisha heshma na sifa ya shule.

Unapofika ripoti kwa mkuu wa shule au makamu mkuu wa shule ili kupewa maelekezo.

**TIPSON M. GIDEON
MKUU WA SHULE**

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

To the officer

.....
.....
.....

From.....

.....
.....
.....

Date

Re.....

Please examine the above named as to his/ her physical and mental fitness for a full time secondary school studies that may also include military training the examination should include the following categories (i-iv) each category for sub – category of which will render the applicants ineligible in case of a defect:

- a) Eye sight
- b) Hearing
- c) Limbs
- d) General diseases
- e) Epilepsy

PART B: MEDICAL OFFICER

(To be completed by a government medical officer)

I have examined the above named and consider that he/ she is physically fit for a full time secondary school studies.

- i. (a) Eye- sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) General diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(E) Epilepsy
- ii. Neuroses
- iii. Other serious diseases.....

DATE **SIGNATURE.....**

STATION **DATE.....**

OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI LWANGWA.

FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI

SEHEMU A:

1. Jina la mwanafunzi
2. Mwaka wa kuzaliwakabila
3. Jina la mzazi/mlezi.....
4. Uhushianokazi yake
5. Anuani ya mzazi/mlezi.....au namba ya simu.....
6. Mahali anapoishi mwanafunzi
7. Umbali kuja shulen ni KM.....

Majina ya ndugu / mlezi mwingine wa karibu

Na.	JINA	UHUSIANO	NAMBA SIMU
1.			
2.			
3.			
4.			

8. Mengineyo (kama mgonjwa, yatima, mlemavu)

SEHEMU YA B: TAMKO LA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LWANGWA

Miminimezisoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule kwamba niko tayari / siko tayari kuzifuata na kwamba sitajihusisha na uchochezi au mgomo wowote katika maisha yangu yote ya shule.

Sahihi ya mwanafunziTarehe

SEHEMU C: TAMKO / AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi ambaye ni mzazi/mlezi waninaahidi kwamba nitatekeleza/sitatekeleza maagizo na mahitaji yoyote ya shule kama nilivyo elekezwa na kwamba niko tayari /siko tayari kushirikiana na uongozi wa shule katika suala zima la malezi na maadili mema ya mtoto wangu kitaaluma na nidhamu yake.

Sahihi ya mzazi/mlezi.....Tarehe

OFISI YA RAISI, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI LWANGWA.

SHERIA NA KANUNI ZA SHULE YA SEKONDARI LWANGWA.

Shule ya sekondari lwangwa inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu ya Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Wewe kama mwanafunzi unapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

- a) Kuheshimu viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi na jamii inayotuzunguka.
- b) Kuhudhuria vipindi vyote vya darasani, pia shughuli za ndani na nje ya shule
- c) Kuwahui shulenii asubuhi na kutekeleza shughuli zinazopaswa kabla ya vipindi
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu juu ya kuwepo ndani au nje ya mipaka hiyo.
- e) Kutunza usafi binafsi na mazingira ya shule kwa ujumla.
- f) Kuvalaa sare ya shule uwapo ndani ya shule na unapo toka nje ya shule.
- g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote, pamoja na maandalio ya jioni (Preparation)
- h) Huruhusiwi kumiliki au kutumia simu uwapo shulenii pasipo idhini maalumu.
- i) Huruhusiwi kwenda bwenini muda wa vipindi pasipo kibali maalumu.
- j) Huruhusiwi kutoka nje ya shule bila kibali kinachoonyesha unapo kwenda na mda wa kurudi.
- k) Huruhusiwi kutumia vifaa vya umeme bwenini au darasani mfano:- Pasi, Hita n.k.
- l) Unapaswa kupanga mstari wakati wa kupokea huduma ya chakula jikoni.
- m) Kuzingatia usafi bwenini kila siku.
- n) Kuepuka lugha ya matusi kwa mtu yeoyote.

MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

- i. Wizi
- ii. Kuto hudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa au utoro
- iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo
- iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi na jamii kwa ujumla
- v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeoyote.
- vi. Kusuka nywele bila kibali cha dini husika na mwongozo wa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
- vii. Kufuga ndevu

- viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevyva
- ix. Uvutaji wa sigara
- x. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa
- xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba
- xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
- xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba mwanafunzi.
- xiv. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
- xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
- xvi. Kudharau Bendera ya Taifa
- xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
- xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi